



**Kila Mwanamke
Anahitaji kufahamu
Kuhusu (PAP Tests)
uchunguzi wa shingo la mfuko
wa uzazi.**

Uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi
huzuia saratani la shingo la mfuko wa
Uzazi Agiza uteuzi wako leo.

PROGRAMU YA
MANITOBA YA
KUKAGUA SARATANI
KWENYE SHINGO
LA MFUKO WA UZAZI



MANITOBA
CERVICAL
CANCER
SCREENING
PROGRAM


CancerCare
MANITOBA
ActionCancerManitoba

Uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi ni nini?

Uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi ni ule unaoweza kupata mabadiliko kwenye shingo la mfuko wa uzazi. Kutibu mabadiliko mapema inaweza kuzuia saratani ya shingo la mfuko wa uzazi.

Shingo la mfuko wa uzazi ni nini?

Shingo la mfuko wa uzazi ni mlango ulio chini ya uterasi. Watoto hupitia hapo wanapozaliwa.

Je ninahitaji uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi?

Ikiwa umeshawahi kufanya tendo la ngono, unahitaji uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi.

Ni mara ngapi nahitaji kufanya uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi?

Wanawake wengi wanahitaji uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi mara moja kila mwaka kwa miaka mitatu. Ikiwa matokeo ni mema, basi unahitaji uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi mara moja kila miaka miwili. Ongea na daktari au nesi wako kuhusu yalio bora kwako.

Je uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi unaweza tambua maambukizo ya magonjwa ya zinaa(STI)?

Lai. Ikiwa uko na wasiwasi ya kuwa umeambukizwa ugonjwa, ongea na daktari au nesi wako.

Ikiwa nimefanyiwa upasuaji wa kutoa chumba cha mtoto – Je, ninahitaji uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi?
Pengine, uliza daktari au nesi wako.

Nimeshafika komahedhi- Bado nahitaji kufanya uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi?

Ndiyo

Ni wakati gani yafaa niache uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi?

Ukishafikisha miaka sabini labla unaweza kukomesha. Ongea na daktari au nesi wako.

Ni lini mwisho nilifanya uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi?

Ikiwa hukumbuki ulipofanyiwa uchunguzi wa shingo la mfuko wa uzazi, piga simu kwa 204-788-8626 au ya bila malipo 1-866-616-8805 au daktari wako.

Ni wapi ninaweza pata maelezo zaidi kuhusu uchunguzi wa saratani ya shingo la mfuko wa uzazi?

Wasiliana na Programu ya Manitoba ya Kukagua Saratani ya Shingo la mfuko wa uzazi kwa nambari: (204) 788-8626 au ya bila malipo: 1(866) 616-8805
www.cancercare.mb.ca/MCCSP: